

MAELEZO SAHIHI

MWONGOZO WA REDIO

# MABADILIKO YA HALI YA HEWA NA MAKAO YETU, DUNIA

## UTANGULIZI

Leo zaidi ya watu bilioni 7 wanaishi duniani. Kila mmoja wetu anahitaji hewa na maji safi, chakula, mavazi, makao, usafiri, rasilimali nyingine na vifaa. Mazingira ya asili hutoa vitu hivi vyote vinavyoendeleza maisha yetu na kuchangia kwa ustawi wetu. Chakula tunachokuza, nishati tunayotumia, madini tunayochimba, vitu tunazozalisha, uchafu na taka zetu hubeba gharama za mazingira na kijamii.

Nyayo ya binadamu duniani imeongezeka zaidi kwa kipindi cha miaka 60 iliyopita. Sasa tunatumia rasilimali na kuharibu mazingira kwa kiwango ambacho tungehitaji ‘ sayari zingine za dunia’ 1.7 ili kuendeleza shughuli hizi (Ecological Footprint Network ). Lakini kama muigizaji Leonardo DiCaprio anavyosema “Tunayo sayari moja tu” (Global Citizen ). Sayansi inatuambia kwamba ni lazima sisi sote tuwaze tabia zetu na madili yetu, ili kupunguza uharibifu wetu duniani na kuendeleza ustawi wa binadamu katika siku zijazo ( Rockstrom et al. 2009).

## UFAFANUZI

- **Mabadiliko ya Hali ya Hewa** ni kinachotokea wakati hali ya hewa ya mataifa inabadilika kwa njia inayoweza kupimwa na ya kudumu. Mabadiliko ya hali ya hewa, baridi au joto la anga linaweza kusababisha mabadiliko makubwa na magumu, kama vile kupanda kwa viwango vya bahari, ukame na mafuriko, ambayo yanaathiri watu, uchumi, jamii na mazingira (NASA, WWF, National Geographic).
- **Kuongezeka kwa joto duniani** ni kinachotokea wakati sayari yetu inaendelea kuwa moto kutokana na mabadiliko ya hali ya hewa. Wanasayansi wengi wanakubali kwamba Dunia iko katika hali ya kupanda kwa kiwango cha joto duniani kinachosababishwa na mabadiliko ya hali ya hewa kutokana na shughuli za binadamu (Earth Hour).
- Watu huchangia kwa mabadiliko ya hali ya hewa na kupanda kwa kiwango cha joto wanapochoma **mafuta za asili** kama vile mafuta, **gesi** na makaa ya mawe; kukata misitu; na shughuli zingine zinazotoa gesi chafu angani. **Gesi chafu** (carbon dioxide au C02 - ambayo ndio gesi kuu kwa zilizo chafu) hutega joto la jua angani, na kusababisha kupanda kwa kiwango cha joto duniani (World Resources Institute).
- **Ecosystems** (mazingira) ni uhusiano uiopo kati ya wanyama, wadudu, mimea, bakteria za udongo, maji, mawe, jua na hewa inayoendeleza maisha duniani. Nishati, virutubisho na taka huzunguka kati ya sehemu tofauti za mazingira, zilizo hai na zisizo hai. Aina tofauti ya mazingira ni kama vile misitu, nyika, majangwa, mito na bahari. Maisha na ustawi hutegemea ardhi yenye rutuba, umbelewele wa mimea, samaki, miti, hewa safi na maji zinazotolewa na mazingira haya (What is an Ecosystem? YouTube).
- **Malengo ya Maendeleo ya Kudumu (SDGs)** hutoa mwongozo kwa binadamu ili wapate afya, ustawi na kufuzu wanapokabiliana na changamoto kubwa duniani, ikiwa ni pamoja na mabadiliko ya hali ya hewa; umaskini na tofauti za usawa kati ya watu; na kusambaratika kwa mazingira. SDGs ni malengo 17 yaliyokubaliwa mwaka wa 2015 na serikali duniani kote, ambazo zinalenga kupunguza nusu ya umasikini kabla ya mwaka wa 2030 bila kupunguza rasilimali za dunia.
- **Mkataba wa Paris** kuhusu mabadiliko ya hali ya hewa ni mkataba wa kihistoria kati ya nchi 195 ili kuzuia uzalishaji wa gesi chafu na kuwekeza katika siku za baadaye - zilizopungua kwa kiwango cha kaboni, ili kuepuka athari mbaya zaidi za mabadiliko ya hali ya hewa. Mkataba huo ulisainiwa

mwishoni mwa 2015 na itaanza kutekelezwa mwaka 2020.

- **Nyayo za Ekolojia** (mazingira) hutupatia njia za kupima athari za kibinadamu duniani - ni kiasi gani cha asili tunacho na tunatumia kiasi gani. Unaweza kutumia chombo cha kuchambua na kulinganisha maisha ya watu ulimwenguni kote, na nyayo za ekolojia za nchi na hata miji mingine (cities). Unaweza pia kuhesabu na kujua changio lako mwenyewe kwenye hali ya mazingira (Personal ecological footprint).
- **Rasilimali ndogo na zinazoweza kuzalishwa upya** (regenerative resources) - Baadhi ya vifaa na rasilimali tunazotumia zinaweza kurejeshwa au kuzalishwa upya, lakini zengine haziwezi.
- **Mafuta, gesi, makaa ya mawe, maji, chuma za kiasili na madini ni rasilimali pungufu na zisizoweza kuzalishwa upya kwa sababu zinatoka kwenye vyanzo ambavyo vitaisha.** Zinaweza tu kujazwa tena baada ya maelfu au hata mamilioni ya miaka (National Geographic).
- **Rasilimali nyingine, ikiwa ni pamoja na miti, mimea, samaki na wanyama, na udongo, huchukuliwa kuwa rasilimali zinazoweza kurejeshwa** kwa sababu zinaweza kuzaliwa upya. Hata hivyo, vyanzo vinavyoweza kurejeshwa bado vinaweza kutumiwa kwa njia isiyodumu - kwa mfano uvuvi mzito au kukata misitu bila kupanda miti tena.
- Rasilimali moja ambayo huweza kurejeshwa ni nishati ya jua. Inaweza kupatikana moja kwa moja kutoka kwa mwanga wa jua, upepo au mawimbi ya baharini (RenewableEnergyForKids).
- Rasilimali zilizo tengenezwa na binadamu ni rasilimali za asili ambazo zimebadilishwa kupitia taratibu fulani. Mifano ya rasilimali zilizo tengenezwa na binadamu ni petroli, makaratasi, plastiki, saruji na teknolojia.

## ONDOA HADITHI POTOFU, PATA UKWELI

| HADITHI | UKWELI |
|---|---|
| **Maisha yataendana na mabadiliko ya hali ya hewa** | Ndio, maisha fulani itatimiza, lakini aina nyingi haziwezi kuponea mabadiliko makubwa na ya ghafla kwenye mazingira yao. Mizingira yote yatabadilika kama mimea na wanyama fulani ambao wanategemeana watakufa (Science Alert). |
| **Afrika imechangia kidogo tu kwa mabadiliko ya hali ya hewa, na hakuna kitu ambacho Waafrika wanaweza kufanya kuhusu tatizo hilo. Kwanini tena tunapaswa kuwa na jukumu la kurekebisha tatizo ambalo weninge duniani kote wameunda?** | Sehemu ya Afrika ya uzalishaji wa gesi chafu ni ndogo sana ikilinganishwa na sehemu nyingine za ulimwengu (Our World in Data). Lakini mabadiliko ya hali ya hewa ni shida ya kila mtu. Vijana Afrika wana jukumu muhimu kwa sababu wakaazi wa miji na idadi ya Afrika inaongezeka zaidi kuliko mahali popote duniani kwa miongo michache ijayo. Bara inakabiliwa na athari kali za mabadiliko ya hali ya hewa (Africa Check). |
| **Hakuna kinachoweza kuzuia mabadiliko ya hali ya hewa** | Kuna hatua zinazoweza kuchukuliwa na watu na taasisi, kama vile kulinda misitu, kutotumia mafuta za kiasili, na kutumia nishati mbadala na mbinu za kilimo zinazo linda mazingira, ili kupunguza kasi cha mabadiliko ya hali ya hewa na kulinda mazingira ya asili iliyobaki, ambayo ni uhai kwetu sote (Guardian). |
| **Mabadiliko ya hali ya hewa ni kuhusu mazingira tu** | Mabadiliko ya hali ya hewa ina athari nyingi kwa jamii, siasa na uchumi duniani kote. Wanawake, watoto na watu maskini mara nyingi huathiriwa na magonjwa na kupoteza maisha kutokana na mafuriko, ukame na athari nyingine zinazohusiana na mabadiliko ya hali ya hewa (BBC). |
| **Mabadiliko ya hali ya hewa itakuwa tatizo wakati ujao tu** | Mabadiliko ya hali ya hewa tayari yapo. Tumepata dhoruba na vimbunga vibaya, mafuriko, ukame na moto za misitu duniani kote mwaka 2018. Viwango vya bahari vinapanda na barafu kutengana duniani kote (NASA). Miji na mataifa zinalazimika kutumia rasilimali zao zaidi kukabiliana na mafuriko na majanga mengine ya asili, badala ya kuwekeza katika kujenga jamii, kama vile kwenye huduma za afya na elimu. |

# JE, WAJUA? (ZA KIMATAIFA)

**JOPO LA KIMATAIFA LA UMOJA WA MATAIFA KUHUSU MABADILIKO YA HALI YA HEWA (IPCC), JOPO LA WANASAYANSI WA HALI YA HEWA INAYO ONGOZA INARIPOTI KWAMBA:**

**Hadi sasa, binadamu wamesababisha kiwango cha degree 1 Celsius ya joto duniani**



**Ikiwa tunaweza kupunguza joto duniani iwe degree 1.5 Celsius badala ya 2 Celsius (ambayo ni kikomo cha juu kilichotajwa), basi mamia ya mamilioni ya watu wanaweza kuepuka kuingizwa katika umasikini uliokithiri unaotokana na hali ya hewa.**



(Guardian)

## UTOAJI GESI LAZIMA UPUNGUZWE HADI UFIKIE SUFURI

**(KUMAANISHA HATUTATOA C02 ZAIDI KATIKA ANGA KUPITA KIWANGO KINACHOWEZA KUNYONYWA) TUFIKIAPO MWAKA WA 2050 ILI 'KUTULIZA' JOTO KWA KIWANGO CHA 1.5 DEGREE CELSIUS**



**70% ya uzalishaji wa carbon dioxide duniani hutoka katika nchi 10 tu**



(World Resources Institute)

**ATHARI ZA MABADILIKO YA HALI YA HEWA:**

**Moja kati ya aina sita za uhai ziko katika hatari ya kutupotelea.**



(WWF)

**Mabadiliko ya hali ya hewa yanayochangia ukame uliokithiri zaidi, mafuriko na dhoruba duniani kote. Hasara za kiuchumi duniani kwa jumla ni dola bilioni $300 kutokana na janga za asili.**



(UN SDG Report 2018)

**NJAA INAONGEZEKA KWA MARA YA KWANZA KWA MUONGO MMOJA. MWAKA WA 2016 KULIKUWA NA WATU MILIONI 815 WENYE NJAA, KUTOKA IDADI YA MILIONI 777 MWAKA WA AWALI.**

| | |
|---|---|
| 2016 | 815 MILLION |
| 2015 | 777 MILLION |

(UN SDG Report 2018)

**Mabadiliko ya hali ya hewa yanatishia kilimo na usalama wa chakula katika sehemu nyingi za Afrika kusini mwa Jangwa la Sahara. Idadi ya watu inaongezeka haraka (kwa mfano, asilimia 80 ya watu nchini Tanzania) wanategemea kilimo na mali asili kwa ustawi wao.**



(UNDP, Climate Change News, Africa Check)

## JE WAJUA? (ZA TANZANIA)

**Tanzania imetia saini makubaliano ya hali ya hewa ya Paris. Nchi ilitoa Mkakati wa Taifa wa Mabadiliko ya Hali ya Hewa mwaka wa 2012 na inashughulikia mabadiliko ya hali ya hewa katika sera kadhaa za kitaifa.**



(Irish Aid)

**Nchini Tanzania, mabadiliko ya hali ya hewa yamekuwa na athari kubwa kwa kilimo, usalama wa chakula na rasilimali za maji. Imekuwa nchi ya 26 inayoathiriwa zaidi na mabadiliko ya hali ya hewa duniani.**



(UNDP, ClimateLinks)

**Tanzania iko katika hali ya hatari zaidi kwa matukio yanayohusiana na mabadiliko ya hali ya hewa, kama ukame na mafuriko, kwa sababu ya kiwango cha juu cha umasikini na utegemezi wa kilimo.**



**Miji inapanuka haraka nchini Tanzania na kuwafanya watu wanaoishi katika makazi yasiyo rasmi wawe katika hatari zaidi ya mafuriko.**



**Ukame uliokithiri mwaka 2005/6 uliathiri mamilioni ya watu na kusababisha gharama kwa uchumi, kiwango cha angalau 1% ya Pato la Taifa.**

(DFID)



## NJIA ZA KUZUNGUMZA KUHUSU MABADILIKO YA HALI YA HEWA

Tafakari maswali yafuatayo, na uzungumze na watu tofauti katika jamii yako (mwalimu, mwanafunzi, mkulima, muuguzi, afisa wa serikali za mitaa, nk.) ili upate maoni tofauti kuhusu mabadiliko ya hali ya hewa:

- Watu wa jamii yangu wanaelewa mabadiliko ya hali ya hewa vipi?
- Katika jamii yangu, watu wanaonaje mabadiliko ya hali ya hewa?
- Je, mabadiliko ya hali ya hewa huathiri makundi tofauti ya watu kwa njia tofauti (yaani wanaume na wanawake, vijana na wazee, wanaoishi mijini na vijijini)?
- Je, mabadiliko ya hali ya hewa inaathiri jamii yangu vipi? Unawezaje kujua kama mabadiliko ya hali ya hewa yanaathiri maeneo mengine ya maisha, kama vile uchumi na afya ya watu?
- Je, jamii yangu inahatarishwa na mabadiliko ya hali ya hewa vipi?
- Ni nguvu gani ambazo jumuiya yangu inaweza kutekeleza ili kujilinda kutokana na athari mbaya zaidi za mabadiliko ya hali ya hewa?
- Jamii yangu inafanya nini ili kukomesha au kuzuia mabadiliko ya hali ya hewa?

## JE, WAJUA? (ZA TANZANIA)

**Idadi ya watu Tanzania inatarajiwa kuongezeka kutoka milioni 56 hadi milioni 130 kabla ya mwaka wa 2050.**

(ClimateLinks)

**Mafuriko katika mji mkuu wa kibiashara nchini Tanzania, Dar es Salaam, unatishia miundombinu ya thamani ya dola bilioni $5.3.**

(VOA)

**Ukosefu wa maji na usafi wa mazingira husababisha vifo 18,500 vya watoto walio chini ya umri wa miaka 5 kwa mwaka, na hugharamia Tanzania $206,000,000 kwa mwaka.**

(World Bank)

**Takriban 85% ya nishati ya Tanzania inatoka kwa kuni na makaa. Sekta hii inaiita mchakato wa kupata nishati kwa kuchoma kuni, na vitu vingine vya kikaboni, *biomass*. Ni 24% tu ya idadi ya watu sasa ambao wanapata umeme, na 42% ya umeme huu unatoka kwenye mabwawa ya umeme, usambazaji ukihatarishwa na ukame.**

(Tanzania Invest)

**75% ya wakaazi mijini nchini Tanzania wanaishi katika makaazi yasiyo rasmi, ambapo kuna hatari kubwa ya ukosefu wa maji, mafuriko na joto kali kutokana na mabadiliko ya hali ya hewa.**

(ClimateLinks)

## NATURAL RESOURCES

Tayari tumezungumza kuhusu mali asili ambazo tunazihitaji kuishi. Hebu tutazame mifano miwili ya vitu tunazo tumia kila siku ili kuona umuhimu wa rasilimali za asili na za kibinadamu kwenye maisha yetu.

**Key** Natural | Human made

| Chakula | | Paper | |
|---|---|---|---|
| **Mboga** | **Nyama** | | |
| Ardhi | Ardhi | Ardhi | Mashine |
| Udongo | Wanyama | Udongo | Kemikali |
| Mwanga wa jua | Maji | Maji | Wafanyakazi |
| Maji | Mwanga wa jua | Mimea | Wahandisi |
| Wadudu | Lishe ya wanyama | Mwanaga wa jua | Ujenzi wa viwanda |
| Bakteria | Dawa | Wadudu | |
| Mbolea | Daktari wa mifugo | Bakteria | |
| Wakulima | Makao | | |
| Wafanyakazi | Wafanyakazi | | |

## NJIA ZA KUZUNGUMZA KUHUSU RASILIMALI ZA ASILI

- Je, ni mali gani asili ambazo jamii yako inategemea? Rasilimali hizi zinasimamiwaje? Rasilimali hizi zinakumbwa na hatari gani?
- Ni nini kinachowezesha au kuzuia watu kutunza rasilimali hizi au kuzitumia kwa njia endelevu?
- Je, rasilimali hizi zinachangia vipi katika maisha ya watu? Maisha ingebadilikaje bila rasilimali hizi?

## DUNIA, MAKAO YETU

Binadamu wako katika familia pana ya viumbe hai, na sayari ya Dunia hutupatia sote makao mazuri. Uhusiano wetu na Dunia ni mpana zaidi ya kuteketeza rasilimali zake. Tunapata uzuri, furaha, maana na hisia ya ustawi tukiwa katika mazingira ya asili. Pia tunapata hisia kamili za upendo, uhusiano na heshima kwa dunia ambayo inatukimu.

Jamii tofauti barani Afrika na kote ulimwenguni zina njia mbalimbali za kuonyesha upendo na heshima yao kwa ulimwengu wa asili, na kuendeleza ujuzi wa kiekolojia ili kuishi kwenye mazingira kwa njia endelevu. Ujuzi huu wa kiekolojia unahifadhiwa katika hadithi na utamaduni (Kanene 2016).

Katika hadithi za jadi, wanyama na mimea mara nyingi huheshimiwa kama wanachama wa familia, na walimu wenye hekima (Behrens 2013).

Je, wajua kwamba:

- Kipepeo anaweza kuonja na miguu yake
- Miti huwasiliana kwa kutumia ishara za kemikali zinazopitia katika mitandao ya uyoga iliyo kwenye ardhi
- Nyangumi huwasiliana kupitia nyimbo ndefu na ngumu ambazo hupitia baharini
- Tazama shairi la mwana-astronomia Carl Sagan 'pale blue dot' mawinguni (YouTube).

## VIDEO ZAIDI ZA KUKUSAIDIA KUTAFAKARI KUHUSU DUNIA:

- Makao yetu (YouTube)
- Prince Ea Man dhidi ya Dunia (YouTube)
- Morgan Freeman kuhusu Suluhisho za Mabadiliko ya Hali ya Hewa (Facebook)
- Wangari Mathai, Mkenya aliyepata taji la Nobel
  Hummingbird video: (Youtube)
  Nobel speech - Wangari Mathai

## NJIA ZA KUZUNGUMZA KUHUSU DUNIA, MAKAO YETU

Maswali ya kuwaza na kujadili:

- Je, kuna maeneo unayotembelea au uzoefu ulio nao unaokufanya ujisikie kuwa karibu na mazingira ya asili? Je, maeneo haya/au uzoefu wako huchangiaje ubora wa maisha yako?
- Watu katika jamii yako wanahusianaje na mazingira ya asili? Je, unadhani watu wanapenda mazingira hayo ya asili? Wanaonyeshaje upendo huu?
- Je, watu katika jamii yako wanashughulikia mazingira ya asili vipi? Unafikiria mila hii/au ufahamu huu umeendelezwaje? Mazoea haya yamekuwa yakibadilika kwa muda?
- Je, watu wanajali hali ya mazingira katika jamii yako? Ikiwa wanaijali, wamechukua hatua zipi ili kuilinda?
- Je, unafikiri kuna umuhimu wa kuendeleza shughuli za kutunza mazingira ya asili katika dunia ya kisasa? Kwa nini ndio, au la?

# MABADILIKO YA HALI YA HEWA NA MAKAO YETU, DUNIA

## MWONGOZO WA REDIO

Mada ya mabadiliko ya hali ya hewa na kutunza dunia ni muhimu sana, na ndio sababu shirika la Children's Radio Foundation inakuhimiza kuiangazia katika vipindi vyako vyote vya redio kutoka sasa. Usiwe na hofu - hatutarajii makala nzima ya mabadiliko ya hali ya hewa na madhara yake kila juma, lakini tunakuomba utengee mada hii nafasi. Inaweza kuwa mwanzo au mwishoni wa vipindi vyako, na tunahisi kuwa: jingle, matamshi mafupi ya kufungua kipengele, taarifa halisi, muundo mmoja wa redio (format) na matamshi mafupi ya kufunga kipengele hicho itatosha. Itakuchukua muda mfupi tu, kati ya dakika 5 na 10.

Kama wanahabari watoto, sote tunajua kwamba tunapozidi kuletea wasikilizaji mada, wanazidi kuwa makini na kuelimika, na hivyo kuchangia pakubwa kuleta mabadiliko!

Tutawashirikisha baadhi ya njia bora za kutenga dakika chache kwa "Dunia, Makao Yetu" katika kila kipindi utakachofanya.

## MIUNDO YA REDIO

Tunaweza kutumia miundo ya redio ili kuunda kipengele cha "Dunia,  Makao Yetu." Tunapendekeza miundo inayohamasisha sauti za wengine na kushirikisha wasikilizaji katika kipindi.

Sauti za Umma, Maoni ya Sauti, Jaribio na Ujumbe wa Sauti kupitia Whatsapp ni njia nzuri za kuwashirikisha wasikilizaji.

### SAUTI ZA UMMA

**Lengo la sauti za umma**
Kupata maoni mengi kuhusu mada moja.

**Unazungumza na nani?**
Mtu yeyote katika jamii.

**Swali**
Je, mabadiliko ya hali ya hewa ni nini?
AU
Kuna athari gani za mabadiliko ya hali ya hewa katika maisha yako na jamii?
AU
Je, wewe unafanya nini ili kukomesha mabadiliko ya hali ya hewa?

### MAONI YA SAUTI

**Nia ya maoni ya sauti**
Kupata maoni ya watu kuhusu mada ambayo wanaijali.

**Unazungumza na nani:**
Vijana na watu wazima katika jamii yako ambao wanaweza kuzungumza kuhusu uzoefu na imani zao za mabadiliko ya hali ya hewa.

## WASIFU WA SAUTI

**Lengo la wasifu wa sauti:**
Wasikilizaji wasikie hadithi ya kuhamasisha kuhusu mada ya kipindi.

**Unazungumza na nani:**
Vijana na watu wazima katika jamii yako wanaokabiliana na mabadiliko ya hali ya hewa katika maisha yao.

## JARIBIO LA KUPIGA SIMU AU KUTUMIA WHATSAPP

**Lengo la Jaribio la Kupiga Simu au kutumia Whatsapp**
Kualika wasikilizaji kushiriki katika fursa inayofurahisha ya kujifunza. Unaweza kuwatuza nafasi ya kutuma salamu au kutembelea stesheni.

**Mtangazaji 1:** Hamjambo wasikilizaji! Unafikiri unayajua yote kuhusu mabadiliko ya hali ya hewa? Hebu tupime ujuzi wako kwa jaribio! Piga simu [TAJA NAMBARI YA STESHENI ] au Whatsapp jibu lako kwa [ TAJA NAMBA YA WHATSAPP]

**Mtangazaji 2:** Sikiza kwa makini. Ni taarifa gani ambayo sio kweli kwa zifuatazo kuhusu Dunia, Makao Yetu?

Dunia inazidi kuwa baridi kwa sababu ya mabadiliko ya hali ya hewa. Tunapoteza aina nyingi za uhai kwa sababu ya mabadiliko ya hali ya hewa na shughuli za binadamu. Kila kitu tunacho hitaji kuishi hutoka duniani.

**Mtangazaji 1:** Piga simu kwenye [TAJA NAMBARI YA STESHENI ] au Whatsapp jibu lako kwa [TAJA NAMBA YA WHATSAPP] na utuambie ni ipi isiyo kweli. Tunataka kusikia kutoka kwako!

## UJUMBE WA SAUTI KUPITIA WHATSAPP

Unaweza kuwakaribisha wasikilizaji mwanzoni wa kipindi chako au kipengele chako cha “Dunia, Makao Yetu” ili watume ujumbe wa sauti kupitia Whatsapp. Kumbuka ni lazima ujumbe wako wa sauti usizidi dakika 1, na uwe katika mada yetu.

Mada hii inaweza kuwa ya tukio au uzoefu wa mabadiliko ya hali ya hewa, wanachofanya wenyewe ili kuzuia mabadiliko ya hali ya hewa, au kile wanachofikiria kuwa ni changamoto kubwa zaidi ya mazingira katika jamii yao.

Kumbuka kucheza ujumbe wa sauti kwa kuufungua na kuufunga vizuri (intro na outro) na pia utaje jina la mtu aliyeyetuma.

**Maandalizi yaliopendekezwa**

[MWANZO:]
**Mtangazaji 1:** Imetimia [TAJA SAA] na tutafanya kitu kipya kwenye [TAJA JINA LA KIPINDI] leo, na kwenye vipindi vingine vifuatavyo. [TAJA JINA LA STESHENI] na [TAJA JINA LA KIKUNDI CHAKO] tunajali makao yetu, sayari hii, na mazingira yetu. Dunia ndio makao pekee tuliyo nayo, na kulingana na ishara ya mambo livyo, hatuitunzi vyema.

**Mtangazaji 2:** Kweli [JINA], kwa hivyo sisi tumeamua kuwajibika kuhusu swala hili katika kila kipindi, kwa sababu tunajali mazingira yetu na tunataka vizazi vijao vifurahie sayari nzuri. Kwa hiyo, karibu kwenye kipengele cha "Dunia, Makao Yetu" kwa muda wa dakika [ TAJA MUDA WA KIPENGELE HIKI, MFANO DAKIKA 5/10] zitakazofuata.

**Mtangazaji 1:** Ndio, moja kwa moja sisi tunaleta majadiliano kuhusu mabadiliko ya hali ya hewa na mazingira yetu - kwa sababu ikiwa tutaiharibu - maisha tunavyoijua haitawai kuwa sawa tena - na sio kwa njia nzuri. Kwa mfano, mabadiliko ya hali ya hewa yanasababisha ukame uliokithiri zaidi, mafuriko na dhoruba duniani kote, na inatishia usalama wetu wa chakula sana. Njaa pia inaongezeka sasa kwa mara ya kwanza katika muongo mmoja!

**Mtangazaji 2:** Kwa hiyo kunawajibika na pia tunakushirikisha kutunza dunia yetu kwa njia bora zaidi sasa. Tukianza kipindi chetu cha "Dunia, Makao Yetu" wiki hii, tutaanza na jaribio kupima ujuzi wako kuhusu mabadiliko ya hali ya hewa.

**Mtangazaji 1:** Piga simu kwenye [TAJA NAMBARI YA STESHENI] au Whatsapp jibu lako kwa [TAJA NAMBARI YA WHATSAPP] au tujibu kwenye mtandao wa Facebook.

Sikiliza kwa makini. Ni taarifa gani zifuatazo kuhusu Dunia, makao yetu, isiyo kweli?

- Dunia inazidi kuwa baridi kwa sababu ya mabadiliko ya hali ya hewa.
- Tunapoteza aina nyingi za uhai kwa sababu ya mabadiliko ya hali ya hewa na shughuli za binadamu.
- Kila kitu tunacho hitaji kuishi hutoka duniani.

**Mtangazaji 2:** Piga simu kwenye [TAJA NAMBA YA STESHENI] au Whatsapp jibu lako kwa [TAJA NAMBA YA WHATSAPP] na utuambie ni gani kati ya hayo yasiyo kweli. Tunataka kusikia kutoka kwako!

Mtangazaji atangaza matokeo ya jaribio na kusherehekea mshindi.

[OUTRO:]
**Mtangazaji 1:** Na hilo linatufikisha mwisho wa kipindi chetu leo. Asante kwa kujiunga nasi, kushiriki kwa kupiga simu na kutu-Whatsapp, lakini hata zaidi ya hayo yote, kwa ajili ya kuleta mabadiliko yako mwenyewe!

**Mtangazaji 2:** Pata [JINA LA KIPINDI] wiki ijayo tutakapo zungumzia mada ingine moto-moto! Na pia endelea kufuata "Dunia, Makao Yetu". Tujitunze, na pia tutunze mazingira yetu. Kwaheri!